



Matunzo ya mtoto katika Mpango wa Kiingereza cha Mtu Mzima Mhamiaji (Adult Migrant English Program)

Je, unahitaji matunzo ya mtoto ili uweze kuhudhuria masomo ya Mpango wa Kiingereza cha Mtu Mzima Mhamiaji (Adult Migrant English Program) (AMEP)? Ukiwa katika darasa la AMEP, matunzo wa bila malipo ya mtoto inapatikana kwa watoto wako walio chini umri wa kwenda shule.

Mtoaji huduma wako wa AMEP atajaribu kupanga matunzo ya mtoto ambayo iko ndani ya dakika 30 kutoka kwa makazi yako au darasa la AMEP. Hii huenda haitawezekana kila wakati. Watoaji huduma wa AMEP watajaribu wawezavyo ili kutafuta kituo cha karibu cha kutunza mtoto.

Watoaji huduma wa AMEP watapanga matunzo ya mtoto inayolingana na mwanzo wa kozi yako ya AMEP. Watajaribu pia kupata matunzo ya mtoto kwa siku utakapokuwa darasani. Wakati mwingine hii huenda haitawezekana kwani maeneo ya kutunza mtoto huwa chache au hukimbiliwa sana. Wakati mwingine, maeneo huenda isipatikane mara moja au unaweza kupewa nafasi kidogo ya kutunza mtoto wakati unapongoja ya siku za ziada kupatikana.

Matunzo ya mtoto ya bila malipo hupatikana tu wakati unapohudhuria masomo ya AMEP. Huwa haipatikani kwa shughuli ambazo ziko nje ya muda wa masomo yako ya AMEP. Wakati hauhudhuria masomo ya AMEP, au kama umemaliza mafunzo yako, utapaswa upanga mpango wako mwenyewe wa matunzo ya mtoto. Kama mtoto au watoto wako hawataweza kuhudhuria matunzo kwa kiwango chochote cha muda, ni muhimu kwamba umwambie mtoaji wako wa huduma wa AMEP. Hii ndipo mipango yoyote ya kuweka nafasi iliyopangwa kwa niaba ya watoto wako inaweza kurekebishwa.

Ukikosa masomo mengi ya AMEP, mtoaji huduma anaweza kubatilisha nafasi yako ya kutunza mtoto. Hata hivyo, ukirudi kwa AMEP, utapata nafasi ya matunzo ya bure ya mtoto tena. Unaweza hata hivyo, kuhitajika kungoja nafasi ya matunzo ya mtoto kupatikana tena.

Wakati unapofanya makadirio ya mahitaji ya matunzo ya mtoto wako, mtoaji huduma wako wa AMEP anaweza kukupa chaguzi mbalimbali ili unaweza kuanza masomo yako haraka iwezekanavyo. . Kwa mfano, unaweza kuombwa:

Matunzo ya mtoto katika Mpango wa Kiingereza cha Mtu Mzima Mhamiaji

- kusoma katika kituo cha jamii kilichoko na mahali pa kutunza mtoto palepale
- kusafiri mbali zaidi kuliko vile unapenda
- kusoma na mwalimu wa nyumbani au kwa njia ya mtandao mpaka nafasi ya kutunza mtoto ipatikane.

Kama mpango wa kutunza mtoto haitoshelezi mahitaji yako, unapaswa kuzungumza na mtoaji huduma wako wa AMEP.

Kwa habari zaidi kuhusu matunzo ya mtoto, tafadhali zungumza na mtoaji huduma wako wa AMEP.